Taarifa ya Kisera – November 2021

Sera za Kodi na Uwekezaji wa Nje wa Moja Kwa Moja (FDI) Tanzania

Tahadhari

Bila mfumo sahihi na sera mpya za kurekebisha dosari zilizipo katika mfumo wa kodi uliopo, itakuwa vigumu kufikia malengo manne muhimu ya kupunguza umaskini, maendeleo endelevu, kushiriki kikamilifu katika biashara kikanda na kimataifa, na kuwezesha wanawake na vijana kiuchumi.

Matamanio

Taarifa hii fupi ya kisera inawasilisha mambo makuu yaliyoibuliwa, na mapendekezo ya utafiti wa kodi, uliolenga kujua namna sera za kodi zinavyoathiri maamuzi ya uwekezaji, kwa wawekezaji wa nje, na mapungufu ya kisera yanayopunguza kiasi cha FDI kinachoingia Tanzania. Utafiti huu unatokana na tafiti za awali pamoja na takwimu zilizokusanywa kwa wadau wakuu wa FDI tangu mwezi Juni hadi Septemba 2021. Mambo yaliyojitokeza yamepelekea kufanya mapendekezo kadhaa ya kuboresha sera za fedha ikiwemo kufanya uchambuzi wa kina wa matokeo ya maamuzi ya kisera yanayoweza kuathiri FDI. Lengo ni kutoa msingi wa kusaidia kuweka sera nzuri za kodi, za muda mrefu, zitakazoweka uwiano mzuri wa kudumisha ukuaji na pia uhimilivu wa uchumi.

Usuli

Kwa zaidi ya miongo mitatu, FDI imekuwa ni mojawapo ya mambo yanayojadiliwa katika jitihada za kukuza uchumi Tanzania. FDI inatumika na mataifa mengi kama mkakti wa kusaidia kuleta mageuzi ya kiuchumi, kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla. Vilevile FDI inasaidia kuweka uwiani mzuri wa urari wa biashara ya nje, kwa kuongeza fedha za kigeni. Hata hivyo, kupata wawekezaji wengi wa nje, si jambo linalotokea tu lenyewe, na wala halipaswi kuchukuliwa kirahisi. Ili kupata wawekezaji wengi wa nje, katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, serikali inapaswa kubuni sera nzuri za uchumi jumla na kuchukua hatua kadhaa za kuvutia wawekezaji. Ubora wa sera zilizopo unatiliwa mashaka hasa kwa kuzingatia mtikisiko uliojitokeza katika mazingira ya kisera na biashara, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

FDI Tanzania, Takwimu

Ongezeko la uwezo wa Tanzania wa kuvutia mitaji ya nje, linajitokeza katika ukuaji mkubwa wa FDI. Tanzania ilipokea mitaji ya nje ya thamani ya Dola za Marekani bilioni moja katika kipindi kati ya 2000 mpaka 2005 ukulinganisha na Dola milioni 70 tu kati ya 1990 mpaka 2000[1]. Ongezeko hili liliiweka Tanzania katika nafasi ya juu ya nchi za Afrika zenye uwekezaji mkubwa wa FDI na ya kwanza katika nchi zizizokuwa na uchumi wa mafuta. Hata hivyo, FDI ilipungua kutoka Dola bilioni 1.5 (kiwango cha juu kilichofikiwa) hadi Dola milioni 846 mwaka 2015, na kuendelea kuongezeka kidogo kodogo kila mwaka kufikia Dola bilioni 1.1 mwaka 2020[2]. Hii ilikuwa asilimia 10 tu ya lengo. Katika miaka ya karibuni sera za kodi zimehusishwa na upungufu wa FDI Tanzania.

Kodi na FDI, Mdahalo Unaoendelea

Athari za sera za Serikali kwa FDI, ni jambo lililovuta hisia za wachumi na watunga sera Tanzania. Sera za kodi zimekuwa zikitumika kama nyenzo kubwa ya kuvutia mitaji ya nje (mfano, viwango vya kodi,

[1] Tanzania Investment Report, 2018
[2] World Bank Report, 2020

vivutio vya kikodi, misamaha ya kodi, kodi ya zuio na unafuu wa kodi). Kumekuwepo na mabishano makali juu ya sera za kodi na namna zinavyoathiri FDI Tanzania.





Source: Tanzania Invest, 2021

Mambo Makuu Yaliyoibuliwa

Tulichambua namna sera za kodi zinavyasaidia kuvutia na kuendeleza kiwango cha FDI Tanzania. Uchambuzi unaonesha kwamba vivutio vya kodi vinaweza kuchochea ongezeko kubwa la FDI katika kipindi cha muda mfupi na muda mrefu. Kumekuwepo na matatizo kuhusu utekelezaji wa sera za kodi, uhimizaji wa watu kulipa kodi, na tafsiri ya maamuzi ya Serikali kuu. Hali hii imesababisha mkanganyiko na kukosekana kwa tafsiri moja mwafaka ya sera hasa katika ngazi za chini. Punguzo la kodi ni nyenzo ya kuvutia FDI Tanzania. Hata hivyo, ili sera ya kodi iweze kuwa na matokeo tarajiwa, ni muhimu Serikali itafute uwezekano wa kupunguza gharama za uzalishaji, kuboresha mazingira ya biashara, na kuleta uhimilivu katika siasa na uchumi jumla. Haya ni mambo makuu yanayoathiri maamuzi ya uwekezaji Tanzania. Aidha, utafiti umeonesha sekta za kilimo, madini, ardhi na majengo zinaathirika zaidi na mitikisiko katika sera za kodi. Kwa hiyo, kupunguza kiwango na wingi wa kodi, na uhimilivu wa sera za kodi, ni nyenzo muhimu za kuvutia FDI Tanzania. Kwa maelezo zaidi tafadhali angalia jedwali katika ukurasa wa 3.

Mapendekezo Makuu

- Kufumua mfumo mzima wa kodi ili kuweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji; pamoja na utaratibu wa kodi unaoamika na himilivu, na hivyo kuboresha ushindani wetu.
- Kupanua wigo wa vivutio vya kikodi ili kujumuisha sekta za kipaumbele na zinazoinukia, zikiwemo ICT, uchumi wa bahari, na kuzingatia wawekezaji katika biashara ndogo, na za kati (small and medium level investors -SMEs).
- Kupanua nafasi na wigo wa vivutio visivyokuwa vya kikodi.

Policy Recommendations

Pengo lililopo	Mapendekezo ya kisera	Matokeo tarajiwa
Kumekuwepo na mabadiliko ya mara kwa mara katika sera ya kodi Tanzania hasa katika kipindi cha miaka 5 iliyopita. Wawekezaji wanataka uhakika, utabirikaji, uhimilivu, na uharaka wa kufanya maamuzi katika taratibu za kodi. Vitu hivi vina umuhimu sawa na kiwango cha kodi kinacholipwa.	Serikali inapaswa kufumua mfumo mzima wa kodi hapa nchini. Uchambuzi wa faida na hasara (cost-benefit analysis) ufanyike ili kuweka uwiano sawa kati ya mahitaji ya serikali na ya wawekezaji.	Kudumisha uhimilivu wa kodi na kuboresha mazingira ya ushindani kikodi Tanzania.
Ukusanyaji mdogo wa mapato ya ndani Tanzania ni kikwazo kikubwa. Changamoto hii inakwaza jitihada za kutoa vivutio vya kikodi vya kutosha kwa ajili ya ukuaji wa uchumi. Uwiano wa wastani wa kodi na ukuaji wa uchumi Tanzania ni asilimia 14 tu ambao ni mdogo sana ukilinganisha na makadirio ya asilimia 25; kiwango kinachotakiwa kwa mahitaji ya maendeleo.	Kubuni sera na mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kulingana na uwezo wa kiuchumi wa nchi.	Wigo mpana wa kodi na kuimarika kwa uwezo wa ukusanyaji mapato ili kulipia mahitaji ya maendeleo.
Ukosefu wa vivutio vya kutosha hasa kukosekana kwa vivutio vya kikodi kama ilivyo kwa nchi nyingine. Vivutio katika viwanda vya magari; maeneo yenye changamoto za usafiri na usafirishaji; sekta za kipaumbele kama TEHAMA, wawekezaji wadogo na wa wastani, na uchumi wa bahari.	Kuanzisha kituo chenye nguvu zaidi ya cha sasa cha uwekezaji (TIC), chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, na kukipa jukumu la kutoa vivutio zaidi kama wanakavyoona inafaa. Pia kupanua vigezo na wigo wa vivutio; Mfano elimu, mambo ya anga, kuwekeza katika mikoa maskini, afya nk. Na kuruhusu vivutio kuendelea kwa wawekezaji wa sasa wakati wanapoweka mitaji mipya katika shughuli zao za sasa. Kuweka ukusanyaji kodi wote katika ngazi ya taifa.	Kupanua wigo wa vivutio kutahamasisha wawekezaji wa nje na ndani katika sekta mbalimbali.
Mtazamo finyu wa vivutio visivyokuwa vya kikodi	Kubuni vivutio sahihi vya kifedha kwa wawekazaji wa nje. Idara kuu ya uhamiaji iangalie uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kuvutia wawekezaji wakubwa kubaki nchini kwa kuwapa vibali vya makazi kwa muda wanaokaa Tanzania.	Kupanua vivuto visivyokuwa vya kikodi ili kuongeza FDI.
Kushindwa kutekeleza mpango wa kutenga maeneo maalumu ya uwekezaji -Special Economic Zones (SEZ) kutokana na kukinzana na sheria ya ushuru wa forodha ya Afrika Mahariki.	Wizara ya Fedha na Mipango iandae na kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya ushuru wa forodha ya Afrika Mashariki.	Hili litasadia utekelezaji wa sheria ya SEZ kuhusu vivutio vya kikodi
Sheria ya uwekezaji ya 1997 inamlinda mwekezaji maalumu, kwa kutamka bayana kwamba, vivutio vya kodi havitabadilika au kurekebishwa, katika njia itakaomuathiri mwekezaji, kwa kipindi cha miaka 5.	Inapendekezwa suala hili liingizwa katika sera za fedha.	Hii itasaidia Serikali kufanya marekebisho kuendana na mahitaji ya nchi ya kiuchumi wakati inapohitajika kufanya hivyo; na itazuia wawekezaji kupata mwanya wa kuishtaki Serikali na kuisababishia hasara.
Mamlaka ya kuidhinisha vivutio vya kodi vya ziada vinavyopendekezwa na Waziri mweye dhamana ya uwekezaji, ya Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji (NISC) ni butu kwani yanakinzana na sheria za kodi. Kuna zaidi ya miradi 19 imeshindwa kupata vivutio vya ziada vilivyoidhinishwa na NISC.	Kuelezea jukumu la NISC kuwa ni kuidhinisha vivutio vinavyopendekewa, kwa maamuzi ya Baraza la Mawaziri (BLM), tofauti na ilivyo sasa yaani kuidhinisha vivutio. Na kuweka mazingira yakayowezesha maamuzi ya BLM kutekelezwa chini ya sheria za fedha.	Maboresho zaidi ya mazingira ya uwekezaji.

Vivutio vya sasa vya kikodi havizingatii umuhimu wa kodi nyingine, kama vile kodi za mishahara, na kodi kwa shughuli zinazoendeshwa bila kuzingatia faida, ambazo kwa sasa zinaangaziwa zaidi kwa upande wa wawekezaji na watunga sera.	Kuongeza wigo wa vivutio vya kikodi ili kujumisha kodi za mishahara na kodi kwa shughuli zinazoendeshwa bila kuzingatia faida.	
Licha ya kazi kubwa ya Serikali na wadau wengine ya kuboresha mazingira ya biashara bado mazingira ya biashara sio rafiki. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na mwongozo wa mazingira ya biashara (Blue Print) na utekelezaji wa mradi wa "BEST-Dialogue".	Kuongeza kasi ya utekelezaji wa "Blue Print". Rejea mapendekezo yaliyotolewa katika Blue Print na kufanya marekebisho kuendana na hali ya sasa ya mazingira ya biashara.	Maboresho ya mazingira ya biashara.
Gharama za kuanzisha biashara na kuziendesha ni kubwa kwani zinajumuisha uwekezaji kwenye miundombinu, kujenga uwezo wa kusafirisha nje, masuala ya kazi, na ushuru wa forodha. Baadhi ya gharama hizi sio za wazi kwa wawekezaji. Wanakutana nazo wanapowalisili nchini, na wakati wa uzalishaji, badala ya kuzijumuisha katika gharama za mradi kabla ya kuanza.	-Kuongeza majadiliano na ushirikiano na sekta binafsi ili kubaini vikwazo vilivyopo katika uanzishwaji wa biashara. -Kutoa miongozo ya wazi kuhusu tozo zilizopo. -Kuhakikisha kuna mfumo mzuri wa uwajibikaji.	Mahusiano mazuri na sekta binafsi yatapunguza misuguano wakati wa kuanzisha biashara. Usahihi na uwazi wa tozo mbalimbali unazuia hisia ya kuonewa na mamlaka za usimamizi na hivyo kuboresha hali kuaminiana. Kuongeza uwajibikaji wa wasimamizi kunapunguza matumizi mabaya ya madaraka na tozo za kiholela.

Mifano halisi ya mambo yanayoweza kuathiri maamuzi kuhusu FDI

- Kodi na ushuru wa forodha katika sekta ya uvuvi Tanzania ni mara tano zaidi ya kiwango kinachotozwa Uganda. Hivyo wawekezaji wengi wa nje katika sekta ya uvuvi wanapendelea kuwekeza Uganda. Aidha, pamoja na kwamba zaidi ya asilimia 50 ya Ziwa Victoria ipo Tanzania, sekta ya uvuvi Uganda ni kubwa zaidi.
- Mzigo wa kodi kwa sekta ndogo ya kilimo cha bustani (horticulture) Tanzania ni asilimia 30 zaidi ya Uganda na mara mbili zaidi ya Zambia.
- Mfanyabiashara anaeuza nje "horticulture" anatakiwa kulipa tozo ya mionzi (radiation fee) ya asilimia 0.2 ya thamani ya hati ya madai. Lakini cheti hiki hakihitajiki na wala hakitambuliki katika soko la kimataifa. Kwa hiyo nchi nyingine washindania wetu wa kibiashara, hawana tozo hii.

Kuna mambo mengine muhimu, ambayo si ya kikodi, yanayoathiri maamuzi; kama:

- Kwa mwekezaji wa nje gharama ya mwanzo ya kuanza biashara Tanzania ni Dola za Marekani 1,000 wakati Rwanda ni Dola 265 tu.
- Aidha, inachukua hadi miezi mitatu kwa mwekezaji wa nje kuanza biashara Tanzania, wakati Rwanda inachukua siku 2 tu.
- Gharama ya maji kwa kiwanda cha nguo Tanzania ni Dola 0.89/m^3. Kenya ni Dola Dola 0.62/m^3 na Ethiopia ni Dola 0.12/m^3.
- Gharama ya umeme kwa kiwanda cha nguo Tanzania ni Dola 0.10/kWh. Ethiopia ni Dola 0.02-0.04/kWh.

Kuhusu mwandishi
Dr. Kaihula Prudensia Bishagazi ni mtafiti, mshauri mtaalamu na mhadhiri katika chuo kikuu cha Mt. Augustine Tanzania (SAUT) katika idara ya uchumi na usimamizi wa biashara. Ni mmojawapo wa timu ya wataalamu wa mradi wa "Pilot4Dialogue" unaotekelezwa na "Tampere Peace Research Institute (TAPRI)" na kufadhiliwa kwa pamoja na Umoja wa Ulaya (EU). Ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa " Avalanche Consultants".